# Imani wakati wa EBOLA





VEM Vereinte Evangelische Mission

ECC CBCA

CBM embracing a broken world through word & deed

ANGLICAN ALLIANCE Development · Relief · Advocacy

# Imani
## wakati wa
# EBOLA



**Imani wakati wa Ebola**
Somo kwa viongozi vya makanisa kwa kuwawezesha kutimiza wajibu wao kwa kuzibiti Ugonjwa wa Ebola

**Somo hizi zilitayarishwa na**

**Isaac Muyonga**, Kiongozi wa Idara ya Afya wa Kanisa la Kibaptisti Katika Africa ya Kati lijulikanalo kama CBCA yaani " Communauté Baptiste au Centre de l'Afrique" kwa kifarasa. Yeye pia ni mwalimu wa Afya ya Jamii katika shule ijulikanayo kama ULPGL yaani "Université Libre des Pays des Grands Lacs" kwa Kifarasa.

**Michael Beasley**, Askofu wa Hertford, Kanisa la England. Michael Beasley ni Askofu Mkuu wa Anglikana wa Hertford katika Dayosisi ya St. Albans (iliyoko kaskazini mwa London huko Uingereza). Pamoja na kuwa kiongozi wa kanisa, yeye kimsingi ni mtaalam wa ile ijulikanayo kama "Epidémiologie" kwa kifarasa, zaidi magonjwa ya kuambukiza. Michael ametoa mchango wake kwa miaka mingi kwenye mipango ya kuboresha afya ya watoto katika nchi nyingi barani Afrika ikiwemo Tanzania, Eritrea na Zambia. Mara kazaa, ameshirikiana na wanamemba wa CBCA kwa kufunza na kuboresha kazi za afya zinazofanywa na Kanisa.

*Muundo*
**Jérémie Ndabo**
jeremiendabo@live.fr | www.ndabodesign.wordpress.com | +243 999 819 862

Goma, RDC | 2020

# YALIYOMO

Ingilio ____________________________________________________ 1

Kipindi cha 1: Kutoka hofu na kufikia tumaini__________________________3

Kipidi cha 2: Kujenga matumaini____________________________________5

Kipindi cha 3: Kuzuia maambukizi kati ya watu, kumutenga mutu kwa sababu ya magonjwa na mazishi ya kukinga____________________________________________________6

Kipindi cha 4: Kuwasiliana wakati wa ugonjwa wa virusi vya Ebola__________13

Kipindi cha 5: Huduma kwa jamii na watu waliopatwa na Ebola___________ 21

# INGILIO|

Inchi yetu nzuri ya Kongo imeshikwa na changamoto nyingi. Vita, umasikini na kutokuwa na utulivu wa kisiasa ni kati ya hali ya maisha ya kila siku katika inchi yetu. Katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, changamoto nyingine ziliongezwa kwa mzigo unaochukuliwa na watu wa Kongo. Mwaka 2018, kuzuka kwa ugonjwa wa Virusi vya Ebola ulianza na umemaliza maisha ya watu zaidi ya1500 mpaka juni 2019, na hadi sasa ishara za kukomesha ugonjwa huu hazija kamilika.

Kuzibiti Ebola ni mojawapo ya vitu vya haraka ambavyo lazima inchi yetu ishugulikie. Kwa kusimamisha maambukizi, kila mtu atahitaji kuleta mchango wake (jamii, wanasiasa, mashirika ya kimataifa na wengine wengi). Jukumu la makanisa katika kuzibiti Ebola ni muhimu. Katika matokeo makubwa ya Ebola yaliofanyika Afrika Mangaaribi kati ya 2013 na 2016, ilikuwa ni wakati waongozi wa dini kuhusika kikamilifu katika jitihada za kuzibiti maambukizi ambayo wimbi la janga hilo limegeukia upande huu wa Kongo. Akizungumuza juu ya kilichotokea pale Afrika ya Mangaribi, mwanachama mmoja wa Umoja wa Mataifa inchini Sierra Leone alisema *"Kushiriki kwa waongozi wa kidini ni wa maana kubadili mchezo."*

### Je!Makanisa yanawezaje kufanya utofauti?

Mchango wa makanisa unafanywa kwa njia tatu kubwa. Ya kwanza, makanisa ni watoa huduma kuu ya afya inchini Kongo. Kupitia hospitali zetu, vituo vya afya na wafanyakazi wa afya tunatoa huduma, msaada na matibabu ya watu walioshikwa na Ebola. Pili, makanisa yetu na viongozi wao ni watu sujaa katika mitaa, vijiji na huaminiwa na kuheshimiwa na raia. Hii inatuwezesha kuwasiliana na waongozi wanaopiganisha ugonjwa huu na kuleta habari za kuaminika kuhusu Ebola ambazo zinahitaji kutumiwa na kila mtu kwa ajili ya kuzibiti maambukizi. Tatu, na muhimu zaidi, tunaweza kuzungumuza na mioyo pia akili za watu tunaowahudumia. Tuna uwezo wa kushughulikia masuala ya hofu, kuchanganyikiwa, mashaka na kuwa na wasiwasi inayoletwa na Ebola. Ni wakati tu mambo haya yatakaposhughulikiwa ndipo maambukizi ya Ebola yatakwisha.
Somo hili limeundwa kwa viongozi wa makanisa inchini Kongo. Ina malengo mawili:

Kukupa taarifa rahisi na iliyo wazi kuhusu Ebola na matendo yanavyohitajika kufanywa ili kuleta maambukizi chini ya uzibiti.

Kukupa somo za kiteolojia zilizochukuliwa kutoka maandiko Matakatifu ambayo itakusaidia wewe, makanisa yako na watu unaowahudumia wafikiri kuhusu masuala ya mila yaliyopo katika jamii ya Kongo ambayo inapunguza uwezo wa kila mtu kufanya kazi pamoja ili kumaliza maambukizi ya Ebola.

# KIPINDI CHA 1: KUTOKA HOFU NA KUFIKIA TUMAINI

### 1.1 Utangulizi: Hofu na Ebola

Agizo gani inarudiliwa sana katika Biblia? Uliza swali hili na watu wataleta mapendekezo mbalimbali ya kile wanachofikiri Bwana anataka tufanye. Mara nyingi ni mshangao mkubwa kwamba agizo ya kawaida ya Mungu ni hii: *"Usiogope".*

Mungu anatuambia mara nyingi tusiogope kwa sababu, katika maisha, kuna mengi ya kuogopesha! Katika Kongo tunazungukwa kila upande na vitu vya kuleta hofu. Kila siku tunaishi katikati ya vita na vurugu, njaa na magonjwa, uzalimu na ugandamizi. Hata hivyo katikati ya hii Mungu anatuambia "Usiogope!" Hii inaweza kuwa nini? Hakika, tunajua kuwa usalama wetu unatoka kwa Mungu ambaye anatupenda na kutuhakikishia sana kwamba majina yetu yameandikwa kwenye vitanga vya mikono yake (Isaya 49:16). Katika karne ya kwanza, Paulo aliandikia kanisa la kwanza la huko Roma, jamii yenye kuwa katika tishio la mateso na shida: "Kwa maana nina hakika kwamba wala kifo wala uzima, wala malaika, wala wenye uwezo, wala maneno ya sasa, wala maneno yatakayokuja, wala yaliyo juu wala yaliyo chini, wala chochote katika viumbe vyote, hakitaweza kututenganisha na upendo wa Mungu ulio ndani ya Kristo Yesu Bwana wetu "(Waroma 8: 38-39). Mungu anatuambia tusiogope kwa sababu hakuna chochote kinachoweza kututenga na yeye na upendo wake.

Hofu imeundwa kwa sababu nyingi. Miongoni mwa hizi sababu, kila mara hofu hutokana na mambo ambayo hatujui, hatuwezi kuzibiti na ambayo hutupa tishio kubwa zaidi. Mara nyingi, hatuwezi kukabiliana na hofu zetu na hii inaweza kusababisha kukataa kile kinachotokea ao kutupia lawama kwa wale tunaofikiri ndio wanaleta vitisho tunavyokabiliana navyo. Tunapofikiria juu ya yote haya, ni rahisi kuelewa ni kwa nini hofu nyingi huzunguka Ebola.



### Maelezo: Ebola ni nini?

Ebola ni virusi, vijidudu (microbe) vinavyoonekana tu kwa njia ya " microscope", vinavyoambukiza mutu na kuanza kuongezeka katika mwili. Katika watu walioambukizwa, Ebola husababisha ugonjwa wa papo hapo, ugonjwa mbaya huu hushambulia viungo vya mwili, huharibu mishipa ya damu, na kuharibu uwezo wa mwili wa kuzibiti joto lake na kusababisha homa. Karibu nusu ya watu walioambukizwa na Ebola hufariki.

Inaeleweka kuwa Ebola iko sasa wakati wote katika mazingira yetu ambamo iko katika wanyama waitwao popo. Inafikia watu kwa kugusa ao kula wanyama ambao wameambukizwa kama popo, makako, nkila, nguruwe ya pori, suala na wanyama wengine wa musituni waliopata magonjwa. Inaongezeka kati ya watu kwa njia ya musongamano, kuwasiliana ao kugusa damu, viungo ao majimaji yanayotoka mwilini mwa watu. Ebola huenea kwa njia ya maambukizi ya binadamu hadi kwa binadamu mwingine kupitia mawasiliano ya moja kwa moja (kwa njia ya ngozi iliyovunjika, iliyo na vidonda ao ngozi [muqueuse] ya ndani ya macho, pua, kinywa, viungo vya uzazi, nk.) na damu au maji ya mwili ya mtu ambaye ni mgonjwa au amekufa kutokana na Ebola, vitu vilivyoambukizwa na maji ya mwili (kama damu, mavi, matapikio) kutoka kwa mtu aliye na Ebola ao mwili wa mtu aliyekufa kutokana na Ebola. Ndiyo maana maziko ya mutu aliyekufa na Ebola ambayo yanarahisisha kugusa mwili wa marehemu inachangia katika kueneza maambukizi.

Wafanyakazi wa afya wanakuwa katika hatari, hasa wakati wanahusika na kutibu (kutunza) wagonjwa wa Ebola ao wakati hawafanye angalisho kwa kutumia kanuni za kujikinga katika hospitali.

Muda kutoka kuambukizwa na virusi mpaka kuanza kwa dalili za ugonjwa ni kati ya siku 2 hadi 21. Mtu aliyeambukizwa na Ebola hawezi kueneza ugonjwa huo mpaka awe na dalili. Watu hubakia kuambukizwa na Ebola kwa muda mrefu kama damu yao ina virusi. Dalili inaweza kutokea kwa gafla na ni pamoja na homa, muchoko, maumivu ya misuli ("muscles"), maumivu ya kichwa na ya koo. Hizi zinafuatiwa na kutapika, kuhara, vipele, dalili za ugonjwa wa figo na maini; Wakati mwingine, kutokwa damu kwa ndani na inje ya mwili (kwa mfano mavi na kwenye ngozi za kufunika meno).

### 1.3 Majifunzo ya Biblia: Kwa kukabiliana na hofu, soma 1 Samweli 17.

Hadisi ya Daudi na Goliati ni hadisi ambayo karibu sisi sote tumejifunza tangu utoto. Lakini, je! umewahi kuisoma kama hadisi kuhusu kukabiliana na hofu?

Hadisi huanza na majeshi ya wafilistini na waisraeli wanaopigana kwenye bonde. Wafilistini wanaamini kwamba ni wa maana sana, wana bingwa asiyeweza kushindwa aitwaye Goliati. Wanaamini kuwa hakuna mtu anayeweza kuwapiga. Goliati anawashawishi waisraeli kutuma bingwa wao. Waisraeli hawaamini kwamba wana mtu yeyote aliye na uwezo wa kazi hii. Je, hali yao ni gani katika mazingira haya? Kama 1 Samweli 17:11 inavyosema, "Sauli na Israeli wote waliposikia maneno ya mfilistini, waliogopa sana na kuwa na hofu kubwa."

**?**

***Swali la majadiliano***

*Soma 1 Samweli 17: 4-7. Kipande hiki kinafafanua kwa nini Goliati anaonekana na kueleweka kuwa chanzo cha hofu kwa waisraeli. Sasa soma sehemu ya Ebola iliyotolewa hapo juu. Kwa nini Ebola inaeleweka kuwa chanzo cha hofu kwa watu?*

Watu wanazeza kujibu kuwa Ebola inaua watu wengi kwa haraka, inakuwa na dalili za magonjwa mengine, nk.

Kuna mwisraeli mmoja ambaye ana uwezo wa kuona mambo tofauti, mvulana Daudi. Katika 1 Samweli 17: 24-27, Daudi anaona mambo mawili. Kwanza, anaona hofu ya waisraeli. Pili, anaona kwamba matokeo tofauti kwa hali hiyo inawezekana. Daudi anaona kwamba Goliati anaweza kushindwa, kwamba yeye mwenyewe anaweza kumushinda. Si kila mtu anayeaminia Daudi. Ndugu yake mkubwa Eliabu anagundua kuwa Daudi anaona mambo namna tofauti na anajaribu kumunyamazisha (1 Samweli 17: 28-30).

**?**

***Maswali ya majadiliano***

*Unajua nini kuhusu Ebola?*

Hakikisha kuwa watu wanajua kuwa Ebola ni ugonjwa wa hatari sana, na kuwahakikishia kuwa siyo pepo wala siasa.

*Una mambo gani ya kusema kuhusu maambukizi?*

*Zungumuzia kupeana mikono, kugusa mugonjwa, kutumia vitu vilivyo ambukizwa, kuwekea watu mikono unapoomba,nk.*

*Ni hofu na wasiwasi gani inayoamka ndani yako?*

*Watu wanaweza kusema juu ya kuenda katika sherehe, kanisani, kupokea wageni, kuenda hospitalini, hofu ya kifo, nk.*

*Watu unaowahudumia wanasema nini kuhusu Ebola?*

*Watu wanaweza kusema juu ya siasa, pepo, biashara ya kimagendo, nk.*

Habari hizi za mtazamo wa Daudi juu ya hali hiyo zilifikia Sauli. Sauli alikuwa na wasiwasi kuhusu uwezo wa Daudi. Lakini Daudi aliweza kumuhakikishia Sauli kwamba Israeli hatashindwa lakini kwamba anaweza kushinda Goliati (I Samweli 17: 31-37). Uaminifu wa Daudi unatoka kwa vitu viwili. Kwanza, uzoefu wake wa kukabiliana na hali ngumu mbeleni. Pili anaweka imani yake kwa Mungu aliye hai ambaye amemusaidia kupitia matatizo mengine katika siku zilizopita.

Sauli anajaribu kumusaidia Daudi kwa kumupa silaha za mfalme. Kwa mwanzo, hii inaonekana kuwa ni wazo nzuri lakini, kwa kweli, silaha ni nzito sana kwamba Daudi hawezi hata kutembea ndani yake! Daudi anakataa vifaa vizito ambavyo ametolewa kwa kukabiliana na Goliati. Badala yake anachagua kukabiliana na sujaa huyu wa wafilistini kwa kutumia vifaa ambavyo vinamfanya aende kwa urahisi.



Kwa mwisho, Daudi alikutana na Goliati (I Samweli 17: 41-58). Daudi alikutana na zarau ya Goliathi. Sujaa wa wafilistini haamini kwamba ana uzaifu wowote unaoweza kuonekana na kijana mdogo na kumuweka katika hatari. Lakini Goliati anajidanganya! Jiwe kutoka kwenye muto lililotupwa kwa imani linawezesha Daudi kushinda Goliati na kukimbiza jeshi lote la wafilistini. Kushinda hofu kwa imani kunaleta ushindi.

**_Maswali ya majadiliano_**

*Swali la majadiliano*

*Kama viongozi wa kanisa, hatuna vifaa na utaalamu wa tiba unaotumiwa na madaktari ili kuzuia Ebola. Ikiwa tunajaribu kuchukua njia hii, tutakuwa kama Daudi aliyejaribu kuvaa silaha za Sauli! Lakini, tuna ujuzi wetu, uwezo na fursa ambazo zinaweza kutuwezesha kutimiza wajibu wetu katika kumaliza maambukizi haya. Je, ujuzi huu unaweza kuwa nini?*

*Watu wanaweza kusema Biblia ao neno la Mungu, ujumbe kutoka Mungu, Roho Mutakatifu, mamlaka kutoka Mungu, nk.*

# KIPINDI CHA 2: KUJENGA MATUMAINI

### Kuelewa Matumaini Kama Mkristo

Tofauti ya hofu ni matumaini. Kama wakristo, tunapozungumuza kuhusu tumaini, hatuseme tu juu ya kutakiana matumaini (kutumaini kuwa mambo yatageuka). Wazo kama hilo la tumaini litakuwa jibu lisilotosha kwa tishio la ukubwa na ugumu sawa Ebola. Tumaini la Kikristo ni kitu pana sana, kirefu na chenye nguvu zaidi. Katika maandiko, tumaini sio tu nia isiyo wazi kwamba kitu kizuri katika siku zijazo kitatokea. Badala yake, ufahamu wa Biblia wa tumaini ni matarajio ya uhakika kwamba mambo mema katika siku zijazo yanakuja. Ni uhakika kulingana na uzoefu wetu tuliyo nao kuhusu wema wa Mungu, upendo wa Mungu, uaminifu ambao ametuonyesha tayari.

Maandiko pia yana wazo kwamba wakati matumaini ni kitu kinachokuja kimsingi kutoka kwa Mungu, pia ni kitu ambacho wanadamu wana sehemu ya kufanya ao mchango wa kuleta. Katika barua kwa Waebrania tunapata maneno yafuatayo: "Mungu sio muzalimu hata kusahau kazi yenu na upendo muliyoonyesha kwa jina lake, kwa kuwa mumetumikia watakatifu na mpaka sasa mungali munawatumikia. Nasi tunataka sana kila mumoja wenu aonyeshe namna ya bidii ile, kwa utimilifu wa matumaini mupaka mwisho. "(Waebrania 6: 10-11)

Kama wakristo, Mungu kwa rehema anatuita sisi kujiunga na kazi ambayo atafanya kwa kuleta matumaini ulimwenguni. Mchango tunaoleta ni muhimu katika kuifanya ndoto kuwa kweli kwa njia ya kazi yetu, upendo wetu, kuomba kwa bidii na imani.

### 2.2 Habari: Njia Kamili za kujenga tumaini wakati wa Ebola

Kuna njia nyingi ambazo tunaweza kutumia kwa kuleta msaada wa matendo wakati wa Ebola. Usaidizi huo huzalisha matumaini ambayo ni zaidi kuliko kuwatakia watu kwa maneno kuwa Ebola itakwisha. Ni tumaini ambalo lina mizizi kwa kuwawezesha watu walete utofauti halisi kwa siku za usoni. Muchango wetu kuleta tumaini hili tunaweza kutumia njia mbalimbali:

### 2.2.1 Kuhimiza na kukubalika kwa huduma (Matunzo)

Kama tunavyojua, kuna sababu za kutosha kwa kuogopa Ebola. Ni ugonjwa mbaya ambao unachukua maisha ya watu wengi. Mbele ya tishio kama hili na hofu ambayo Ebola inaleta, jibu la kawaida na linaloeleweka kabisa ni "kukana". Wakati tunakabiliwa uwepo wa Ebola, kama wanadamu tunaweza kwa namna fulani kufikiri tunaweza kujikinga kwa kukataa kukubali kinachotokea. Katika hali hii mara nyingi inamaanisha sisi tunakataa msaada wa huduma za matibabu ikiwa wanatusukuma kukubali

**Maswali ya majadiliano**

*Je, unaelewaje neno 'tumaini'? Unazani ina maana gani kwa watu unaowahudumia? Unajibuje kwa wazo kwamba tumaini ni kitu ambacho Mungu na sisi tuna sehemu ya kufanya?*

kuwa kitu kibaya kimefika katikati yetu. Watu wanaweza kufikiri kama :"Ikiwa sioni daktari," ni kusema, hakuna kitu kitakachoweza kutokea kwangu."

Kama hivyo ndivyo watu wanafikiri wakati wa Ebola, ni hatari sana. Ni hatari kwa watu ambao wameambukizwa na virusi na kwa watu wanaoishi karibu nao ambao wanaweza kuambukizwa na wagonjwa. Kama viongozi wa kanisa, faraja na msaada wetu unaweza kuwa wa muhimu katika kuwasaidia watu tunaowahudumia kutafuta na kukubali uchunguzi, matibabu na chanjo katika vituo vya afya wakati vinahitajika.

Kugundua Ebola ni kazi ya ujuzi kwa watu wa afya (Daktari). Dalili za Ebola zinafanana sana na maambukizo mengine kama malaria, homa ya "typhoide" na "meningite". Hivyo tu kwa sababu mtu ana homa haimaanishi kwamba ana Ebola (inaweza kuwa matokeo ya sababu nyingi). Kwa hiyo ni muhimu sana kuzibitisha kwa njia ya "Laboratoire"kuwa dalili mutu anazoonyesha zinasababishwa na Ebola.

Kwa upande wa matibabu, watafiti katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) juu ya Ebola wametangaza maendeleo ambayo yamefikia kugundua dawa mbili zitakazo wapa wagonjwa nafasi nzuri ya kupona. Lakini huduma za kukabiliana na dalili kama upungufu wa maji huboresha maisha. Maendeleo katika matibabu yanafanywa wakati wote na aina nyingi za matibabu zinaweza kupimwa.
Chanjo mpya kwa kujikinga na Ebola inashuhudiwa sana kuwa na uwezo wa kulinda watu na maambukizi.

**2.2.2 kuzuia maambukizi ya virusi**
Tuna haki ya kuzungumuza juu ya kuzuia maambukizi ya virusi wakati tunaweza kuonyesha kikamilifu kwamba watu waliopata magonjwa haya hutendewa kwa heshima na ubinadamu. Ni wakati watu wameuona upendo wetu wa kweli kwa matendo ndipo watasikiliza maonyo tunayofanya kwamba wanapashwa kubadili tabia zao na jinsi wanavyoishi kila siku.



Kwa kuzuia Ebola, lengo la shughuli zote ni kupunguza hatari ya uambukizi kutoka binadamu hadi binadamu mwengine kwa njia ya mawasiliano ya karibu na watu wenye dalili za Ebola, hasa kwa maji yao ya mwili. Njia bora ya kuzingatia hii katika maisha ya kila siku ni kutoa vifaa kwa ajili ya kuosha mikono mara kwa mara kwa milango ya kuingilia mahali ambapo watu wanakusanyika pamoja katika jamii (makanisa, shule, katika majengo ya serikali, katika hoteli, nk.).

Kama viongozi wa kanisa, hatua ambazo tunahitaji kuchukua katika nafasi yetu ya huduma ya kichungaji inaelekea maeneo mawili ya shughuli zetu.

Matembezi ya kutoa huduma kwa watu walioambukizwa na virusi vya Ebola lazima yafanywe chini ya uongozi, usimamizi na maelekezo ya wafanyakazi wa matibabu wenye ujuzi. Hii inaelekea kuvaa vifaa vya kujikinga binafsi wakati wa kutembelea wagonjwa hospitalini. Kuosha mikono mara kwa mara huhitajika baada ya kutembelea wagonjwa katika hospitali, na baada ya kuona wagonjwa nyumbani.

Mazishi ya heshima na yenye kukinga ni sehemu ya pili inayohitaji ufahamu wa mbinu za kazi, uelewa na huruma (Ona somo lingine kuhusu mazishi).

## 2.3 Majifunzo ya Biblia: Matumaini yanayojengwa katika Mungu

Maombi inahitajika kuimarisha kazi zetu zote katika eneo la Ebola, kama yanavyofanywa katika kila sehemu ya kazi yetu. Kupitia maombi tunajifungua wenyewe kwa nguvu za Mungu zinazofanya kazi ndani yetu. Kupitia maombi Mungu hutubadili na kutujenga kuwa watu ambao anataka tuwe. Kwa njia ya maombi tunaalika matendo ya Mungu ndani na karibu na sisi kwa uponyaji na matumaini. Kupitia maombi tunakua katika tumaini na imani kwa Mungu.

Soma Isaya 43: 1-7
Sehemu hii ya maandiko kutoka Isaya inazungumuzia watu wa Mungu waliochukuliwa wakati wa uhamisho wa Babeli. Wao ni watu ambao hali mbaya zaidi imetokea: inchi yao imeshindwa, jiji lao Yerusalemu limeanguka na wamepelekwa kufanya kazi ya kulazimishwa katika taifa la mbali. Mambo yote walioogopa yamefika. Wanaonekana kuwa hawana chochote cha kutarajia na hakuna mtu wa kuamini. Hata hivyo katika hali yao Mungu analeta ujumbe wa upendo na uhakika na huwapa watu ahadi ya ukombozi na kurudi makwao. Ujumbe wa Mungu unaweka ndani ya watu hawa hali ya matumaini ambayo yanatimizwa wakati wao wanarudi Israeli wakiwa wamewezeshwa kuishi tena kama watu wa Mungu wa heshima, wa huruma na kweli.

?

***Maswali ya majadiliano***

*Umejuaje uaminifu wa Mungu wakati wa shida katika maisha yako? Maombi yako inakuambia nini kuhusu uaminifu wa Mungu? Jinsi gani, sisi waongozi wa kanisa, tunaweza kuonyesha watu waliopatwa na Ebola kwamba wanaheshimiwa na kupendwa na Mungu (v4). Unazani 'ukombozi' ungeweza kumaanisha nini wakati wa Ebola? Watu wanaweza kusema kuwa ukombozi ni kumaliza magonjwa, kuwa na hakika kuwa Mungu yuko pamoja nasi, kuendelea na mafundisho katika kila kizazi, nk.*

# KIPINDI CHA 3: KUZUIA MAAMBUKIZI KATI YA WATU, KUMUTENGA MUTU KWA SABABU YA MAGONJWA NA MAZISHI YA KUKINGA



### 3.1 Mwili umetakaswa na Mungu

Ndani ya imani yetu ya Kikristo tunafahamu kwamba miili ya wanadamu imetakaswa na Mungu. Katika mwanzo, Mungu aliumba mwanadamu kwa sura yake (Mwanzo 1:26). Katika uumbaji huu wanadamu wanafanywa kuwa wa kiroho na wa kimwili. Kwa hiyo miili yetu ni ya muhimu sana kwa nafsi yetu. Kwa kweli, mojawapo ya musimamo wa Kanisa wakati wa mwanzo ilikuwa kukataa mawazo ya wale waliosema kwamba kitu pekee ambacho kilikuwa muhimu ni roho zetu na kwamba lengo la maisha ni kutarajia kuondoka katika miili.

Kwa wakristo, mwili ni wa muhimu sana. Tukumbuke kuwa wokovu wetu unazungumuza kuhusu Mungu kupata mwili. Katika Yesu, Mungu anatwaa mwili ambayo kwa kweli ina maana 'katika nyama za mwili'. Mungu huweka takatifu na hubariki miili yetu kwa kuwa ndugu yetu katika Yesu Kristo. Katika maandiko ya Paulo, miili yetu inaelezwa kama "hekalu ya Roho Mtakatifu" (1 Wakorintho 6:19) na watu wa Mungu wanaokusanyika pamoja wanaelezwa kama 'mwili wa Kristo' (1 Wakorintho 12:27). Wakati Yesu anaweka agano jipya ambayo tunapashwa kukumbuka, alichukua mfano wa mwili (mkate) na anasema juu yake 'Huu ni mwili wangu'.

Umuhimu wa mwili unaonekana katika maelekezo mengi ambayo andiko linatoa juu ya kile tunachofanya na miili yetu kuhusu kuiweka safi, kuhusu kuchunga afya, kuhusu jinsi tunavyoitumia kwa upendo

kwa kulinda uhai. Miili yetu inafanya kazi kubwa kuelewa sisi ni wanani. Inatutengeneza na kupunguza yale tunaweza kufanya na kufikia. Hatari kubwa ya miili ni kwamba hatimaye itafikia mwisho, na kutufanya tufe. Miili yetu inatufafanua kama binadamu na ni ya maana sana kwetu.

Kwa sababu miili yetu ni ya maana sana, haishangazi kuona namna tunavyoitunza kuchunga afya, kuhusu jinsi tunavyoitumia kwa upendo na tunavyoitunza hata inapokufa, ni swala la muhimu sana kwa watu wote wa miaka yote. Mazishi ya heshima imekuwa ya msingi kwa utambulisho wa kibinadamu, inaonekana tangu zamani kuwa watu wanahakikisha kuwa wamezikwa vizuri. Hii kuzikwa vizuri inatofautiana kutoka kwa mila moja na ingine na wakati mumoja kwa mwingine. Katika kila mila, watu wameweka taratibu wazi kuhusu jinsi mazishi yanapashwa kufanyika. Ukiuliza mchungaji yeyote wa kanisa namna ya kuwa na shida na familia ao jamii wakati wa kuzika mutu atakuambia ni kuzika vibaya (tofauti na mila yao).

### 3.2 Ebola na Kugusana

Kwa kuwa wanadamu wanaishi katika miili, kugusa ni muhimu sana kwetu. Tunagusana kila mmoja ili kuonyesha upendo, huruma na uhusiano. Ikiwa mtoto ni mgonjwa ile anayohitaji ni kuchukuliwa katika mikono ya wale wanaomupenda. Wakati mtu anapofariki, mara nyingi mawasiliano ya mwisho tunayoweza kuwa naye ni kugusa mwili wake ao sanduku kabla ya kuenda kaburini. Ushawishi wetu wa kibinadamu wakati tunafariji mtu katika huzuni ao kila aina ya mateso ni kumugusa. Sasa tukumbuke kuwa moja ya ubaya na ukali wa virusi vya Ebola ni njia ambayo hufanya kugusa kuwa hatari. Ebola huambukizwa na kuwasiliana na binadamu, damu au maji ya mwili wa mtu ambaye ana ugonjwa ao amekufa kutokana na Ebola. Inaambukizwa kwa kugusa vitu ambavyo vimeharibiwa na maji ya mwili (kama damu, mavi, matapikio) kutoka kwa mtu mgonjwa wa Ebola. Inaweza kupitishwa kwa kugusa mwili wa mtu ambaye alikufa kutokana na maambukizi.

Kwa sababu ya hili, Ebola inatuweka kwenye mgongano kati ya kile tunachopashwa kufanya ili tuwe salama na kuzuia maambukizi ya virusi ambayo ni kugusa (Usiguse, wakati njia hii ndio inaonyesha undani wa usaidizi kwa mtu aliye na mahitaji). Vichwa vyetu vinatuambia jambo moja, mioyo yetu inatuambia jambo lingine. Mvutano tunaoishi unaongezeka wakati tunapoona hatua za kuzuia maambukizi ambazo zinachukuliwa na wale wanaohusika na kuwajali watu wanaoishi na Ebola ao mazishi ya wale waliokufa kutokana na virusi. Hakuna hata mmoja wetu anayeweza kuchagua kuona jamaa kutengwa na muuguzi (Infirmière) aliyevaa nguo kamili za kufunika mwili kwa kujikinga. Hakuna hata mmoja wetu atakayejitolea kuzikwa katika mfuko wa plastiki uliofunikwa. Sio kitu cha kushangaza kuona kwamba watu waliopatwa ao kuishi katika maeneo yanayo kabiliana na Ebola wanakataa utumiaji wa mifuko ya plastiki kuzika wafu wao. Hata hivyo tahazari hizo ni za maana sana kama tunataka kuzibiti (kushinda) ugonjwa huu wa Ebola. Kutafuta njia kati ya mawazo ya watu na ukweli kutoka kwa moyo ni mojawapo ya changamoto kubwa zaidi kwa viongozi wa kanisa ili muchango wao uwe na matokeo mazuri kwa kuzibiti ugonjwa huu.

***Maswali ya majadiliano***

*Unajua hatua gani zinazohitajika kuchukuliwa ili kuzuia maambukizi ya Ebola?*

*Watu wanaweza kutaja kunawa mikono na sabuni ao majifu, usafi wowote (choo, mazingira, chakula), kuenda kwa hospitali mapema kujua unaugua na nini, kupata chanjo,nk.*

*Je! Haya hufanya ujisikie namna gani?*

*Unazani unaonekanaje na watu wa muji ao kijiji chako unakotumikia unapochukua hatua za kuzuia maambikizi ya Ebola?*

*Watuwanaweza kusema wanaonekana kama wale waliopokea rushwa, wale wanaosaidia adui wa raia,nk.*

## 3.3 Kuzuia maambukizi kati ya watu

### 3.3.1 Matendo ya Kanisa

Kiwango kikubwa ambacho viongozi wa kanisa wanaweza kuchukua ili kusaidia kuzuia usambazaji wa ugonjwa kwa binadamu ni kuhakikisha kuwa vifaa vya kuosha mikono vinatumika na kutumiwa na kila mtu anapoingia kwenye majengo yote ya kanisa na kwa kila chumba cha mikutano ao huduma mbalimbali.

Wakati wa ugonjwa huu, maombi ya uponyaji yaepuke kuwekwa mikono. Mbele ya kushiriki meza ya Bwana, watu watumie madawa ya kuua virusi kwa mikono. Watu wawe makini kwa kupunguza maambukizi wakati wanapobatiza kupitia maji mengi ao kugusa watu wanaobatizwa. Neno hili linahitaji utafiti zaidi.

### 3.3.2 Kuwasiliana Kanisani

Ni muhimu kukumbuka kuwa dalili za Ebola ni sawa na zile za maambukizi mengine kama vile malaria ao "typhoide". Haiwezekani kumwambia mtu kama ana Ebola tu kwa kuwaangalia. Maambukizi yanaweza kusibitishwa kwa kufanya vipimo vya uchunguzi vinayofanywa katika "laboratoire". Wakati wa Ebola, kila mtu akiwa na dalili kama vile homa, kutapika au kuhara hupaswa kuhimizwa kupimwa katika kituo cha afya (ama kupunguza uwezekano wa kuambukiza wengine, ao kupata matibabu na huduma ya haraka iwezekanavyo). Ni muhimu kuweka mukazo kwamba wakati wamoja hutafuta kukataa ukweli wa Ebola ao uwezekano wa kuambukizwa, hakuna mtu anayejiponya kwa kufanya hivyo.

### 3.3.3 Kumutenga mutu

Katika hali ngumu inayoonyesha ao kuleta wasiwasi kwamba mtu ameambukizwa na virusi, kunahitajika mutu huyu atengwe kwa siku 21, baada ya hapo hatakuwa na hatari kwa watu walio karibu naye.

Kutengwa ukiwa na magonjwa yanayohatarisha maisha ni muda wa kutisha sana. Kama ilivyojadiliwa mbeleni, haiwezekani kwa wapendwa wa mutu aliyetengwa na wanamemba wa kanisa kumutolea huduma ambayo kwa kawaida hutolewa kwa mtu mgonjwa wa kawaida. Hata hivyo, mtu aliyetengwa bado anahitaji kujua kwamba anapendwa, wanamujali na kumuombeya. Mawazo mapya yanahitajika katika kila mazingira ili kuwezesha huduma hizo kutolewa. Kutoa neno, maombi na njia nyingine za kuruhusu watu waliyotengwa kujua kwamba hawakusahaulika ni muhimu. Utunzaji pia unapashwa kupanuliwa kwa wale walio na jukumu la kuhusika na wale waliotengwa ili waweze kuendelea kutoa heshima, msaada na tahazari kwa wale walio katika mahitaji kiafya.

### 3.3.4 Kuzika na ukingo

Kama ilivyojadiliwa, tamaduni zote duniani zimeweka namna wao wenyewe watafanya mazishi kwa kuonyesha heshima, huruma na kumtunza mtu aliyekufa na wale ambao wamepona ugojnwa. Wachungaji wote wanajua kuwa ni muhimu kusikiliza jamaa wakati wa kilio na mazishi. Ebola husababisha changamoto kubwa kwetu katika eneo hili kwa sababu maambukizi yanaweza kupitishwa kwa kugusa mwili wa mtu aliyekufa kutokana na virusi. Matokeo yake hufanya tabia nyingi ya mazishi kuwa si salama.

Matukio ya watu wanaozaniwa kuambukizwa na Ebola huweka wachungaji mahali pagumu. Kwa upande mmoja kuna matumaini kwamba tunapashwa kufikia matarajio ya kitamaduni ya wapendwa kuhusu jinsi mazishi yanapashwa kufanyika. Kwa upande mwingine tunahitaji kufanya mazishi kwa njia ambayo hailete maambukizi zaidi, ugonjwa na kifo. Njia pekee kupitia mvutano huu ni kufikiri kwa uangalifu na kwa uaminifu kuhusu njia za kufanya mazishi vizuri kama zinavyoweza kuwa katika mazingira ambayo yanakubalika. Kwanza kuna kazi kubwa ya mawasiliano kuelezea jamaa na jamii ya mtu ambaye amekufa vinyume vinavoletwa na kifo cha Ebola, na namna ambazo mazishi yanaweza kutolewa kwa njia iliyo salama kwa kila mtu. Pili, ndani ya vinyume ao vikwazo vilivyopo, kuna haja ya kuhakikisha kwamba mazishi hayatakuwa kama kawaida. Maneno ya huduma ya kawaida ya mazishi inapashwa kubadilika. Makaburi yanapashwa kuwa na urefu unaofaa kuepuka maambukizi. Mahitaji ya kuzika miili katika mifuko ya kinga lazima ielezwe kwa upole.



**_Maswali ya majadiliano_**

*Taja matendo ambayo wewe na kanisa lako munaweza kufanya ili muweze kuzuia mambukizi ya Ebola.*

*Watu wanaweza kutaja kuweka vyombo vya kunawa mikono kwa mulango wa hekalu, muchungaji kuwa mufano kunawa mikono na kupata chanjo, kuleta juu ya Ebola katika mahubiri, kusikiliza kanisani ushududa wa mutu aliyepona Ebola, kuleta vikundi wya uhamasishaji jkatika mikutano ya vikundi kanisani ao nyuma ya ibada.*
*Unataka uzungumuze na nani kusudi mawazo haya yatekelezwe? Kanisa lako linawezaje kuwa na mpango wa utekelezaji unaojulikana na kila mtu?*

### 3.4 Majifunzo ya Biblia

Kufikiri kwa makini kuhusu zoezi za kidini zinazoambatana na ugonjwa unaoambukizwa kwa kugusa sio jambo jipya. Wakati ambapo Biblia iliandikwa, ukoma ulieleweka kuwa ni ugonjwa unaosababishwa na kugusa, ambao uenezaji kupitia idadi ya watu unaweza kuzuiwa ikiwa hatua zinazofaa zilichukuliwa.
Soma Walawi 13: 1-8

Maagizo ya Walawi yaliyotolewa katika sehemu hii ya Maandiko yana mengi sawa na matendo mazuri kuhusu Ebola.
Kwanza, wakati mtu anaonyesha dalili za kuwa na maambukizi (v2), kitabu cha walawi ni wazi kwamba mtu aliyepatwa na ugojwa asifiche ao kukataa kile kinachotokea. Badala yake ataletwa kwa Haruni kuhani ao kwa mmoja wa wanawe makuhani.
Amri walizopewa walawi zinaonyesha kwamba dalili zozote zinahitajika kuwa swala la utambuzi wa makini na kupimwa (vv3-4). Maandiko yanaonyesha kwamba sio maambukizi yote yanayofanana. Hii ni sawa kusema kuwa matukio ya homa ambayo inaweza kusababisha Ebola, inaweza kuwa dalili ya ugonjwa mwingine kama vile malaria ao "typhoide". Vipimo vinavyofaa pekee ndivyo vinaweza kuonyesha kama homa inaletwa na nini kusudi mutu apate matibabu yanayofaa.

Maelekezo katika kitabu cha walawi hutumia pia kwa makini kutengwa kwa mugonjwa. Mustari wa 5 huzungumzia mtu aliyegonjwa kuwa amefungwa na kuhani kwa siku saba. Kutengwa huko kunapendekezwa kama njia bora ya kuzuia maambukizi ya ugonjwa huo. Baada ya siku saba, uchunguzi zaidi umeamriwa ili kuhani atambue kama maambukizi yamepita ao la (v6). Kama maambukizi yamekwisha, mtu hutangazwa kuwa safi, tayari kurudi kwenye maisha ya kawaida ndani ya jamii.

Walawi 14: 1-9
Kitabu hiki cha walawi kinaendelea kutoa maagizo juu ya kuamua kama mtu anaambukizwa ao la. Pia inatambua kwamba baada ya mtu kupitia katika kipindi cha magonjwa, anahitaji kuingizwa tena katika maisha ya jamii. Na hii hufanyika kwa ibada ya wazi na ya watu wengi inaonyesha kwamba wote sasa ni pamoja na mtu aliyeambukizwa na kwamba hawapati hatari kwa yeye ao mutu mwengine. Ibada ya watu wote ilijulikana katika utamaduni ao mila ya waisraeli wakati ule. Kisha Ibada ilihusisha kunyunyizia mtu aliyepona damu ya ndege iliyotolewa sadaka na kisha mpango wa kumuosha na kumunyoa. Kama wakristo, hatutumii mila ya ibada ya Agano la Kale. Lakini tunapashwa kuzingatia haja ya watu ambao wamepatwa na maambukizi ya kuingizwa kwenye jamii na kuonyeshwa kwa watu wote kuwa wao ni salama.

***Maswali ya majadiliano***

*Taja matendo ambayo wewe na kanisa lako munaweza kufanya ili muweze kuzuia mambukizi ya Ebola.*

*Watu wanaweza kutaja kuweka vyombo vya kunawa mikono kwa mulango wa hekalu, muchungaji kuwa mufano kunawa mikono na kupata chanjo, kuleta juu ya Ebola katika mahubiri, kusikiliza kanisani ushududa wa mutu aliyepona Ebola, kuleta vikundi wya uhamasishaji jkatika mikutano ya vikundi kanisani ao nyuma ya ibada.*
*Unataka uzungumuze na nani kusudi mawazo haya yatekelezwe? Kanisa lako linawezaje kuwa na mpango wa utekelezaji unaojulikana na kila mtu?*

# KIPINDI CHA 4: KUWASILIANA WAKATI WA UGONJWA WA VIRUSI VYA EBOLA



### 4.1 Changamoto za mawasiliano

Kiongozi yeyote wa kanisa anajua kwamba mawasiliano ni moja wapo wa sehemu ngumu sana za kazi yetu. Ni mara ngapi umezani umeleta mara kwa mara habari kwa wanamemba wa kanisa na unawasikia wakisema 'hakuna mtu aliyewahi kuniambia kuhusu jambo hili!'

Ikiwa mawasiliano juu ya mambo ya kawaida katika kanisa ni ngumu, basi kuzungumuza kuhusu Ebola lazima iwe ngumu zaidi. Kutokea kwa ugojwa huu kwa gafla hutoa changamoto nyingi kwa mawasiliano mazuri.

Ya kwanza, Ebola inaleta hofu. Ni magonjwa yanayoleta mauti na kila mtu anataka kuyaepuka. Watu wengi hawana habari kuhusu ugonjwa wenyewe (namna unavyoenea, namna gani kujikinga, tiba inapatikana namna gani). Wakati maswali ya watu hayapate majibu, ni kawaida kugeukia habari za fununu kwa kuamua nini itafanyika. Tangu zamani, hofu ya ugonjwa inaleta kila aina ya uvumi juu ya jinsi ya kuepuka maambukizi na namna ya kupata matunzo. Tunaamini haraka yale yanayopendekezwa, hata kama hayana msingi halisi wa kile kinachosemeka, kwa sababu tunaweza kujisikia kwa urahisi kukosa nguvu ya kujiponya na tishio la Ebola na kutaka kuizibiti kwa nguvu zisizo halahi.

Ya pili, Ebola inatokea katika mazingira ambamo tayari kuna mashaka mengi na kushitakana kati yetu. Kuna mashaka na wasiwasi kwamba inatokea kwa sababu za kisiasa na kutokusikilizana katika serekali. Kuna mashaka ya wanamgambo na vikundi vya waasi wanaotumia silaha ambavyo mara nyingi vimewatesa watu. Kuna mashaka ya watu kutoka inje ambao wanakuja kusaidia kuzibiti ugonjwa huu unaowaua watu, wakati hakuna kuaminiana kati ya serekali na raia. Hata watu wa nia nzuri kutoka inje wanashindwa kuelewa masemi ya watu wa maeneo yanayokumbwa na ugonjwa kwa hivi nguvu ya kuhamasisha watu kuepuka ugonjwa inakuwa ndogo. Katika hali hiyo, maswali yanayoulizwa ni kama yafuatayo: 'Watu

hawa wanajiwazia kuwa wanani? Kwa nini wamekuja huku kwetu? Je, kwa kweli wanakuja kutusaidia ao wanakuja na sababu nyingine? "Katika hali hiyo ambamo uaminifu ni mdogo ni vigumu sana kuleta ujumbe juu ya kutokea kwa ugonjwa ambao kila mtu atakubali na kuamini.

Katika hali hii, viongozi wa kanisa wana sehemu muhimu kuleta jibu kwa maswali ya watu. Kanisa huishi ndani na karibu na jamii wanazozitumikia. Wao hawana nia ya kuwa na watu kwa muda mufupi yaani kuwa hapa leo na kuondoka kesho. Kiongozi wa kanisa, hata kama yeye ni sawa na mtu mwingine yeyote ule, anajulikana kuwa katika jamii kwa manufaa ya watu anaowahudumia. Katika huduma yake, anaonyesha upendo na heshima na kufanya kila kitu na uaminifu. Wakati Ebola ilipotokea Afrika ya mangaribi kati ya 2013-2016, maneno ambayo raia wa Sierra Leone walisema pamoja na viongozi wao wa kanisa yalikuwa kama ifuatavyo: Tuko watu wa kuaminika, wa kumucha Mungu, wa kuheshimiwa, wa kujitolea, waaminifu, wenye busara, wa ujasiri na ushauri.Na sisi viongozi vya makanisa katika R D Congo , tuige mufano wa watu wa Sierra Leone, tuaminiane katikati yetu , tuseme neno moja, tushirikiane kwa ku piganisha janga hili.

Hakuna mtu anayesaidiwa katika hali mbaya kama kuzuka kwa Ebola kwa kuamini habari ambazo ni sahihi ao zisizo za kweli. Inawafanya wale wanaozisikia na kuzipokea kuwa kama 'mtu mjinga aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga' (Matayo 7: 26-27). Changamoto kwa viongozi wa kanisa ni kuleta mafundisho ya kweli na ambayo yatasaidia wale wanaoyasikia kuwa kama 'mtu mwenye hekima aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba' (Matayo 7: 24-25). Ni wakati tunaweza kusimama juu ya mwamba wa ukweli ndipo itakuwa rahisi kuzibiti ugonjwa wa Ebola.

### 4.2 Majifunzo ya Biblia

Mawasiliano katika mazingira ya kutokuelewana

Kuzungumuza na mamlaka na ukweli sio rahisi. Ni changamoto kwa kusikilizwa vizuri na kuna mengi ambayo yanafanyika kinyume na mawazo yetu mema. Hii ilikuwa kweli hata kwa Yesu! Katika huduma yake alikabiliana na uadui, shaka na watu kukataa kabisa kushirikiana na kile alichosema. Ikiwa tunapashwa kusema ukweli juu ya Ebola, tunapashwa kutarajia changamoto hizi pia na tunapashwa kuwa na utayari wa kukutana nazo.

Soma Marko 3: 19b-35

Sura ya tatu ya injili ya Marko imeandikwa katika mazingira ya huduma ya Yesu anayeponya magonjwa. Katika v1-6 Yesu anamponya mtu mwenye mkono uliopooza. Katika vv7-12 amefundisha umati mkubwa na akafanya uponyaji kati yao. Katika mstari wa 13-19 aliwaita mitume kumi na wawili kumusaidia katika huduma yake.

Lakini pamoja na kazi hizi zote nzuri, katika vv19b-27, Yesu anakabiliwa na upinzani kutoka kwa njia mbili. Ya kwanza ni kutoka kwa familia yake. Unaweza kufikiri kwamba wanaelewa kwa urahisi kile Yesu anachofanya na wangependa kufanya kazi naye na kumsaidia. Hata hivyo wanaonekana wamekosa uhakika. Wanafikiri anajihusisha na mambo ambayo hapashwi kufanya. Watu wanasema mambo mabaya kuhusu huduma ya Yesu ('Ameruka akili v21) na kwa sababu hiyo familia yake' ilikwenda kumuzuia 'v21.

Kundi la pili kupinga Yesu ni waandishi. Nia yao ni kutafuta kumuzaraulisha Yesu. Wao hutoa uvumi ambao hutafuta kuuliza kila kitu anachokifanya na kuleta madai ya kwamba kazi ya Yesu haikuwepo kwa wema lakini kwa uovu. 'Yeye ana Beelzebuli na kwa uwezo wa pepo huwafukuza pepo', wanadai waandishi.

Yesu anakabiliana na vikundi vyote, waandishi na familia yake. Angalia jinsi anavyofanya. Yesu hawambii kuwa wao ni wajinga ao kama wanafanya makosa. Kufanya hivyo ingekuwa tu kuanzisha ubishi usiyoleta matunda yoyote. Yesu anajaribu kuchukua watu kwenye mambo mengine ya majadiliano ambayo inaweza kuwasaidia kutafakari kwa mtazamo tofauti juu ya maoni yao na ufahamu wao. Kwa waandishi,Yesu anawauliza swali la filosofia lililowashirikisha kwa mazungumuzo: 'Ni nani anayeweza kushinda uovu na kufanya mema ambayo ninafanya kwa njia ya uovu?' Anaongeza, 'Shetani anawezaje kumfukuza Shetani?' (V23).

Kwa familia yake, Yesu anawaalika kumujua yeye na utimilifu wake: munanijua, anasema, 'munajua kwamba ni lazima nifanye jambo jema, hata kama hamuwezi kukubali hilo. Kufanya mapenzi ya Mungu ni muhimu zaidi kwangu kuliko yale munayofikiri. Na mukisimama na kuanza kufikiri juu yake, mutatamani kufanya kazi pamoja nami, sio dhidi yangu. Yesu anasema, "Yeyote anayefanya mapenzi ya Mungu ni ndugu, dada na mama yangu." (V35)

?

***Maswali ya majadiliano***

*Huduma ya Yesu ya uponyaji ilikuwa kinyume na mawazo ya familia yake, viongozi wa kidini na waandishi. Ikiwa wewe na kanisa lako unashiriki katika kutafuta kushughulikia Ebola, unafikiri watu wanaweza kusema nini kuhusu wewe?*

*Watu wanaweza kusema umepewa rushwa, umenunuliwa, umekuwa mmoja wa wale walionunuliwa, unafurahiya mateso ao vifo vya watu, unajitajirisha juu ya damu ya wengine. Ni nini watu wanasema kutoka ndani ya kanisa na nini watu wanasema kutoka inje? Kutoka ndani ya kanisa, watu waaweza kusema Kiongozi ameharibu kanisa, anapenda pesa na amepewa pesa. Wengine kutoka inje ya kanisa wanaweza kusema ni mwisho wa dunia, ni munyama, ni kusahau kazi yake, ni kusumbukia mambo ya dunia, nk. Je, mambo yote yatakuwa mazuri ao utapata upinzani fulani?*

*Watu wanaweza kusema si wote watakaokubaliana na muchungaji, wengine wataendelea kuamini habari za uvumi.*

*Ikiwa upinzani unakuja, unazani utachukua sura gani?*
*Watu wanaweza kusema kushikilia kweli, kutafuta mbinu za kuelewesha watu na hekima, kusikiliza kila mutu, nk.*

*Unawezaje kujiandaa ili uweze kujibu upinzani wowote, kama vile Yesu alivyowajibu wale waliomshtaki?*

*Watu wanaweza kusema kujihakikishia una habari kamili kuhusu ugonjwa, kuwa na muda wa kuomba, kuchunga uhusiano muzuri na raia, nk.*
*Unawezaje kuwawezesha ili mazungumzo yasiwe juu ya upinzani na mapambano lakini kuhusu fikira, kuleta mawazo na majadiliano?*

*Watu wanaweza kusema kuwa na hekima, kuwsikiliza watu, unyenyekevu, kusikiliza watu, nk.*

Soma Luka 7: 18-23

Yohana amebatiza Yesu na anaona Roho Mtakatifu akishuka juu yake (Luka 4: 21-22). Pamoja na hili, kama Injili inavyoendelea kusema, inaonekana kwa mwisho wa maisha kwamba Yohana bado ana shaka juu ya Yesu ni nani na yale aliyokuja kufanya. Anawatuma wanafunzi wake wawili kumwuliza Yesu "Je, ndiwe atakayekuja ao tunapashwa kutarajia mwingine?" (Luka 7: 19-20).

Inaonekana kwambaYohana anafikia kufanya hivyo kwa sababu kuna hadisi nyingi zinazotofautiana kule inje juu ya Yesu ni nani na mambo anayoyafanya. Kati ya haya mambo kuna yale yaliyo ya manufaa kwa Yesu lakini mengine yanaenda kinyume na ujumbe wake. Je, Yesu anakabilianaje na changamoto ya utofauti uliopo? Mutu anaweza kufikiri kuwa atajibu kwa kuzungumuzia mamulaka aliyo nayo kwa kusema 'munapashwa kuniamini, Mimi ni Mwana wa Mungu!'. Lakini Yesu hakufanya mambo haya yote. Badala yake anawaonyesha wanafunzi wa Yohana kile anachofanya: kuwezesha vipofu kuona na walemavu kutembea, nk (Luka 7:22). Yesu anajua kwamba matendo yanasema kwa sauti zaidi kuliko maneno na kwamba kile anachofanya ni ujumbe bora wa kuzungumuza wazi juu ya ukweli anaouchukua. Mambo haya yanafika pia kwa sisi?

***Maswali ya majadiliano***

*Maswali ya majadiliano*

*Namna gani kazi zako za kupiganisha Ebola zitakuwa zaidi ya kuwazungumuzia kuhusu ugonjwa huu?*

*Watu wanaweza kusema kuwa mufano kwa kuchunga kanuni za afya, kuleta vifaa vya usafi, kuhudumia wagonjwa na jamaa zao, kuwapokea wliopona, nk.*

*Kanisa lako linaonyeshaje kwa Matendo yake kwamba Ebola ni kweli, na kwamba tunahitaji kuipiganisha kwa matendo?*

*Watu wanaweza kusema linapoweka vifaa vya kunawa mikono mbele ya hekalu, kutumia dawa ya usafi wa mikono mbele ya meza ya Bwana, kuzungumuzia Ebola kanisani, nk.*

*Unafikirije watu katika muji wako wataitikia namna gani huduma unayowaletea?*

*Watu wanaweza kusema kuwa watafuata mufano wako, utahitaji kuwashirikisha na kuwapa habari za kweli.*

*Huduma hiyo itawasaidiaje kuinua ufahamu wao?*

*Watu wanaweza kupendekeza kuwazungumuzia katika vikundi vidogovidogo, kuwaletea watu waliopona ili wafanye ushuhuda.*

## 4.3 Kusema ukweli juu ya Ebola kwa mamlaka na usahihi

Katika Injili ya Yohana, Yesu anasema "Kama mukikaa katika neno langu, ninyi ni wanafunzi wangu kweli. Nanyi mutajua kweli, na kweli itawaweka ninyi huru". Changamoto kwa viongozi wa kanisa wakati wa Ebola ni kutumia mamlaka yetu ya kuaminika katika jamii ambazo tunatumikia kusaidia watu waelewe ukweli kuhusu kuambukizwa ili ugonjwa ulioko sasa uweze kumalizwa. Changamoto yetu ni kusema ukweli na kusikiwa ukisema ukweli. Ni kuwasaidia wale ambao kwa njia ya hofu ao sababu zingine zisizojulikana wanaleta maneno yasiyo na msingi ili sisi sote kama jamii tuje pamoja na kuchukua musimamo utakaotusaidia kumaliza huu ugonjwa kati yetu.



Uwezo wetu wa kusema ukweli unaweza kuimarishwa na matendo mengi:

Huduma tunayoleta ifanyike kwa heshima. Hakuna yeyote kati yetu anayefurahi akiitwa vibaya, kuwa mujinga ao asiye na akili, hata kama inaweza kuwa kweli. Kama tulivyosema katika majifunzo ya Biblia kuhusu Marko 3 hapo juu, wakati Yesu anapokutana na kutoeleweka juu yake mwenyewe na kazi zake, hakupambana na wale wasiomukubali. Angefanya hivyo, ingekuwa amemwaga petroli kwenye moto unaowaka na kufanya mambo kuwa mabaya zaidi. Badala yake alipata njia za kujihusisha kwa uaminifu na wale ambao hawakubaliani naye, kuingia katika majadiliano ambayo yanawezesha mawazo kuchunguzwa na kubadilishwa.

Tunaweza kusema ukweli na uhakika wakati tunapoelewa vizuri kile tunachokizungumuzia. Kwa hiyo, fikiria wakati wote kuelewa Ebola kama vile mtu yeyote asiye Daktari ao muuguzi (infirmière). Inua uwezo wako wa kujibu kama inavyofaa maswali ya watu juu ya kuzuka kwa Ebola, namna mutu anavyoipata, wapi inatoka, namna ya kuizuia, nk.

Uwezo wetu wa kujibu maswali na wasiwasi za watu huimarishwa wakati tunaweza kuwaambia watu sio tu kile wengine walituambia, lakini wakati tunaweza kuzungumuzia yale tuliyoyaona. Kwa hiyo tumia kila njia iwezekanayo kukutana na wataalamu ao madaktari wa eneo yako ili kuona kile wanachokifanya na jinsi wanavyotaka kuzibiti kuzuka kwa ugonjwa huu. Hii itakuweka kwa nafasi nzuri kuwa imara na kukataa kwa upole maoni mabaya na ya uongo juu ya shughuli za afya na kuwawezesha watu kuamini kazi zinazofanyika kuzibiti ugonjwa. Nia yako pia itakuwa ya faraja kubwa kwa wale wanaofanya kazi katika huduma za afya, itakuwezesha wewe mchungaji kuwaombea na kuwahubiria neno.

Yesu ana mamlaka ya kuzungumuza katika maisha yetu kwa sababu alishiriki kikamilifu katika kila hali ya maisha yetu ya kibinadamu kwa kuwa mmoja wetu. Yeye hazungumuzi nasi kutokana na mtazamo

wa inje juu ya hali yetu. Anazungumuza kama mshiriki kutoka ndani. Tunahitaji kukamata mufano huu ikiwa tunataka kuleta mchango wetu katika kuzibiti Ebola. Tunapata haki ya kuzungumuza juu ya kuzuka kwa Ebola wakati tunaweza kuonyesha kikamilifu kwamba watu wanaozuia matunzo ya wagonjwa, wale wanaowaficha, wale wanaokimbia chanjo wanafanya vibaya na wanaweka taifa katika hatari. Matendo haya yatasema zaidi kuliko maneno tunayoweza kusema.

***Maswali ya majadiliano***

*Maswali ya majadiliano*
*Unahitaji kufanya nini kwa kusema na uhakika pia na mamlaka juu ya Ebola?*
*Watu wanaweza kusema uwe na habari kamili kusuhu Ebola*

*Unahitaji matendo gani kwa ajili yako na kanisa lako ili kuwezesha hili kutokea?*
*Watu wanaweza kusema kupata mafunzo, kushindikizwa na vifaa vya kazi, nk.*



# KIPINDI CHA 5: HUDUMA KWA JAMII NA WATU WALIOPATWA NA EBOLA



Ugonjwa na maambukizi, kifo na kupona ni hali halisi ambayo sisi sote tunajua sana. Kwa mfano, hakuna hata mmoja wetu anayeshangaa kupatwa na malaria ao magonjwa fulani ya tumbo (minyoo) kwa sababu ya kuwa nayo kila mara kati yetu, tunaona mambo haya kama sehemu za maisha ya kila siku. Tunajua jinsi ya kukabiliana na magonjwa hayo; Hata kama tunaelewa hatari yake, hatuwezi, kwa ujumla, kuyaona kama sababu za hofu. Lakini, Ebola ni tofauti sana. Kwa karibu kila mtu, maambukizi ni kitu ambacho hajawahi kupata. Kama watu binafsi ao jamii, hatuna ufahamu ao ujuzi fulani tuliotumia mbeleni kwa kukabiliana na maambukizi. Kwa hivi, kila mtu anatafuta ukweli na majibu, na inaweza kuwa vigumu kupata habari zilizoaminika na kuhakikishwa.

Katika hali kama hiyo, uvumi na habari zisizo na musingi zinazunguka kwa urahisi. Kwa sababu tunajua kwamba Ebola inaua, maambukizi yanaleta hofu kubwa. Mambo haya yote hufanya mchanganyiko mbaya ulio kama sumu ambayo huzalisha hisia mbalimbali kwa watu binafsi na jamii waliopatwa na Ebola. Hisia hizi ni pamoja na hofu, wasiwasi, hasira, kuchanganyikiwa, kukata tamaa, nk.

?

***Maswali ya majadiliano***

*Je! Unajisikia namna gani unapojaribu kutoa huduma na muelekeo (uongozi) katika kukabiliana na kutokea kwa Ebola?*

*Watu wanaweza kusema unasikia woga kwa sababu unapata upinzani zaidi katika mazingiza ya usalama mudogo.*

*Je! Ni magumu makubwa gani yaliyokupata wewe?*

*Watu wanaweza kutaja kulaumiwa na kusingiziwa kwamba umepata pesa, kuonekana kama mutu asiyeamini anayefanya kazi katika ushirikiano na pepo wabaya.*

*Ni hatua gani za maana unazoziona zimefaa kwa kuchukuliwa mahali ulipo sasa?*

Watu wanaweza kutaja kuleta usalama, kuboresha uhusiano kato ya waongozi wa mupango wa kupiganisha Ebola na raia, kuheshimu kanuni za afya, kuhimiza raia kuenda haraka kwenye kituo cha afya wanapokuwa na daili za ugonjwa, nk

## 5.1 Wajibu maalum wa viongozi vya Kanisa

Kama viongozi wa kanisa, michango mizuri ambayo tunaweza kuleta kwa kuwezesha huduma bora kwa watu waliopatwa na Ebola ni mbili: Kwanza, tuna jukumu la kufanya kwa kuwezesha jamii kukabiliana na mripuko wa maambukizi. Tunahitaji kuleta ufahamu ambao unawahimiza watu kuunga mkono wale waliopatwa na maambukizi, siyo kuwakataa. Tunahitaji pia kusaidia jamii kudumisha mawasiliano kati ya watu inayowawezesha kufanya kazi pamoja na kuleta mchango wetu katika kuhakikisha kwamba umoja unadumishwa bila kuzoofika kwa kukabiliana na kutokea kwa Ebola.

Pili, tunahitaji kuwapa watu binafsi waliopatwa na Ebola (wale walioambukizwa na wapendwa wao) huduma ambayo itawasaidia wakati wanapoambukizwa kwa kukubali matokeo yake ambayo inaweza kuwa kufariki ao kuishi.

### 5.1.1 Kutunza Jamii

Kama viongozi wa kanisa, njia bora zaidi ambazo tunaweza kuunga mkono ndani ya jamii zetu ni kushughulikia hofu na kulaumiwa zinazojitokeza mahali kuliko Ebola na kuonyesha kuwa huduma ya watu waliopatwa na Ebola inawezekana, inaweza kuwa salama kama inavyotarajiwa.

#### 5.1.1.1 Kupunguza Hofu

Kuhusu swala la kukabiliana na hofu, mchango wetu bora ni kuwa na uwezo wa kujiamini na kujihakikishia kuendelea kusema ukweli juu ya Ebola. Ya kwanza ni kwamba hii ni maambukizi ambayo yanahitaji kuzibitiwa haraka, na kwamba Ebola inaweza kumalizwa kama kila mutu analeta mchango wake katika hatua zinazohitajika kuizuia. Pili, ni muhimu kuendelea kusema kuwa wale ambao wamepona ao kutoka mahali walipotengwa kwa kufanya uchunguzi hawaambukizi tena na hawana hatari yoyote kwa jamii. Watu kama hao wanahitaji usaidizi wa jamii na hawapashwi kutupiliwa ao kuonyeshwa vidole.

#### 5.1.1.2 Kukabiliana na kulaumiwa

Kuondolewa kwa lawama husaidia uzibiti wa Ebola ao huduma ya watu waliopatwa na ugonjwa huu. Kulaumu ni matokeo ya watu kuwasheta vidole wagonjwa ao wale waliopona. Kwa mwisho hii husababisha aibu, kujificha na kutokuwa na uwezo wa kushiriki waziwazi na kwa urahisi katika hatua zinazohitajika kuzuia Ebola ao kujibu maambukizi wakati yanapotokea.

Iwapo lawama inapunguza nguvu ya kuzibiti maambukizi, inaonyesha ukweli kwamba kwa watu wengi, ni njia ya kusema kuwa Ebola ni ugonjwa wa hatari na hii ni asili ya kibinadamu. Watu wanataka majibu kwa nini kitu kama Ebola kinatokea. Mahali ambapo habari na uelewa ni mdogo, inaeleweka (ingawa hakika haifai) wakati watu wanajaribu kuleta sababu za kuzuka kwa maambukizi zisizo na msingi. Kati ya vyanzo vikuu vya uvumi vinavyosababishwa na kulaumiwa ni kwamba maambukizi husababishwa na njama za watu wabaya, ao zambi za watu (ni azabu ya Mungu kwa watu binafsi kwa matendo yao mabaya) ao uchawi (unafanyika na mutu mumoja na kuleta ubaya kwa watu wengi). Kujibu kwa kila sababu hizi kunatuletea changamoto kubwa.

Habari za kufanyiwa njama zinatokana na kutorizika kwa watu na ukweli wa habari (au ukosefu wa habari) ambazo zimewasilishwa kwao juu ya Ebola. Kama ilivyojadiliwa katika kipindi cha kuwasiliana katika mazingira ya Ebola, mahali ambako hakuna maelezo yanayotosha, kunatokea habari nyingine zinazotengenezwa na watu. Kama tulivyosema, njia bora ya kuachana na hizi habari za uongo ni kutoa habari za kweli na hakika, kuleta maelezo kamili juu ya kutokea kwa ugonjwa, sababu zake na maendeleo ao hatua zinazohitajika kuuzibiti. Kwa kufuatana na mawazo ya watu kuhusu uhusiano kati ya zambi na ugonjwa, ni lazima kujua kuwa kwa maoni ya watu wengi, uhusiano huu haukubaliki. Maandiko Matakatifu yenyewe ina mawazo tofauti sana kuhusu jambo hili.

Mashairi mengi yanayosibitisha uhusiano huu yanapatikana katika Agano la Kale. Mwanzo inasema kwamba kifo kilikuja ulimwenguni kwa kutokutii kwa Adamu na Hawa (Mwanzo 3). Mahali pengine (kama vile 2 Samweli 12) ugonjwa na kifo huonyeshwa kama matokeo ya moja kwa moja ya vitendo vibaya vya mtu. Kwa upande mwingine, Yesu mwenyewe hakufanya uhusiano wowote kati ya zambi na ugonjwa, badala yake alikataa kwamba hakuna uhusiano (angalia Yohana 9: 2-3; Luka 13: 1-5). Zaidi ya maoni ya Maandiko, tunaishi katika ulimwengu ambamo mbinu za kisayansi zinakataa uhusiano wowote kati ya maadili ("morale") ya mtu na maambukizi yake kwa Ebola. Wakati huo huo, kwa watu wengi tunaotumikia, kushikilia wazo la uhusiano huo kunaleta uvumi juu ya kitu ambacho kinaonekana kuzidi uwezo wetu.

Kwa njia nyingine, kuna watu wamoja ndani ya jamii ambao wanatumia mawazo ya uchawi kwa kueleza kwa nini wamoja wanapata ugonjwa na wengine hawaupate. Lakini wengine wanakataa kabisa mawazo haya.

Kwa mawazo yoyote yaliyopo, kujibu Ebola kunahitaji mupango wa haraka. Kwa wakati huu, ni muhimu kutambua kwamba changamoto yetu ya haraka ni kutumia muda murefu kwa kuelewesha jamii kuhusu kujikinga na Ebola. Ni lazima tupate njia na ufahamu pamoja na watu wa mahali kunakotokea ungonjwa kwa kutumia mbinu zinazokubalika na kufanya kwa haraka ugonjwa huu uzibitiwe bila kungoja.

?

***Maswali ya majadiliano***

*Maswali ya majadiliano*

*Kwa nini unafikiri kwamba kwa watu wengine ni muhimu kusadiki kuwa zambi na ugonjwa ao uovu na ugonjwa vinahusiana?*

*Watu wanaweza kusema kuwa kuna magonjwa yanayotokana na zambi (1 wakorinto11,30), lakini mengi ni kwanjia kawaida kwa kutokuheshimu kawaida ya afya.*

*Kama* kiongozi wa kanisa na mkristo, unawezaje kufanya kazi bora namna gani ili kusaidia jamii kupiganisha Ebola kwa haraka kati ya watu walio na ufahamu tofauti kuhusu uhusiano wa zambi na ugonjwa?

Watu wanaweza kutaja kuwaelewesha Mandika Matakatifu, kufanya kazi katika uhusiano na watu wa afya, kuwapa watu mafunzo ya afya.

### 5.1.2 Kutunza watu binafsi waliopatwa na Ebola

#### 5.1.2.1 Utunzaji wakati wa maambukizi

Mtu aliyeambukizwa na Ebola anakabiliwa na changamoto kubwa sana. Kati ya haya ni pamoja na usumbufu mkubwa wa kimwili wa kuwa mgonjwa mahututi, kutengwa na maeneo ya kawaida na watu, mushtuko wa kuzungukwa na wahudumu (Daktari,muuguzi,nk.) wanaovaa mavazi ya kinga, hofu ya kifo yenyewe, nk. Watu wa jamaa la mugonjwa watapata shida nyingi pia, ikiwa ni pamoja na hofu ya kifo, wasiwasi kwamba mtu huteseka mahali asipopendwa ao kati ya watu wasiomujua, wasiwasi juu ya maisha ya familia baadaye, kutengwa na majirani na wasiwasi kuwa walioishi na kuwasiliana na mugonjwa wanaweza kuwa wameambukizwa.

Changamoto ya kichungaji ni kufanya kila kitu ambacho kinafaa kwa kushikilia mtu aliyeambukizwa (paomja na familia yake) katika jamii inayofanya huduma kwa upendo upande mumoja, pia wasiwasi na kumbukumbu mbaya upande mwingine. Mafikiri mapya yanahitajika ili kuhakikisha kwamba mtu aliyetengwa kwa sababu ya Ebola anajua kwamba hakusahaulika na kwamba familia yake na jamii hawakumusahau, wanafikiri juu yake, wanamuombea. Mawazo mapya yanahitajika pia kuwasaidia watu wa jamaa ya yule aliyeambukizwa kuleta usaidizi unaofaa ili kufanya kazi za nyumbani, kuwasikiliza na kuwatunza katika mazingira ya wasiwasi mkubwa, kuwaletea majibu yenye nguvu ambayo yanawasaidia kukabiliana na tabia mbaya ya kushetwa vidole na majirani.

#### 5.1.2.2 Utunzaji baada ya kupona

Matokeo ya Ebola ni kwamba mtu hufa ao anashinda maambukizi. Mtu aliyekufa anahitaji kuzikwa kwa ukingo na kwa heshima iwezekanavyo. Kama tulivyosema katika kipindi cha tatu, kuhakikisha ukingo na heshima pamoja wakati wa Ebola kunahitaji mawazo mazuri na mawasiliano bora kati ya wote waliohusika yaani wafanyakazi wa afya na jamaa.

Mtu anayeshinda maambukizi ya Ebola anakabiliwa na changamoto nyingi. Kwa muda fulani atakuwa muzaifu kimwili kwa sababu ya mazara ya maambukizi. Musaada unaofaa kimwili, kisaikolojia na kiroho unahitajika kwa yule aliyekuwa mugonjwa na kwa familia yake. Wakati huo huo kuna changamoto ya kuponea chupuchupu. Hii inaomba huduma ya kumusikiliza na kuzungumuza naye.

Mtu aliyeshinda maambukizi na familia yake ana uwezekano wa kukabiliana na kushetwa vidole. Kutakuwa na wasiwasi kuwa yeye ataambukiza wengine akikaa katikati yao. Kunaweza kuwa uvumi kuwa magonjwa yao ni hakikisho kwamba wao ni watu wabaya waliolengwa na pepo wabaya. Kazi ya mchungaji na wakristo wote ni kuonyesha upendo kwa kuwakumbatia wale waliopona ugonjwa. Hii inamaliza matendo yote ya kuwalaumu na kuwasheta vidole ao kuwakataa.

**Maswali ya majadiliano**

*Leta matendo ambayo kanisa lako linaweza kufanya kuhudumia watu waliopatwa na Ebola pamoja na jamaa zao.*
*Watu wanaweza kutaja kuwapokea kwa furaha, upendo wa ndugu, kuwapa nafasi ya kufanya ushuhuda, kwasaidia kisaikologia, kiroho na kivitu, nk.*

*Watu gani wanaweza kuhusishwa kwa kufanya huduma hii?*
*Watu wanaweza kutaja waongozi wa kanisa na wakristo waaminifu.*

*Wanaweza kuhitaji mafunzo gani kwa kufanya kazi hii?*
Watu wanaweza kutaja mafunzo yanayofaa kuhusu ushauri (counseling)

## 5.2 Majifunzo ya Biblia

Soma Yohana 11: 1-44
Yohana 11 inaeleza hadisi ya kifo cha Lazaro na kufufuliwa kwake na Yesu. Maandiko haya yanaweza kusomwa kwa njia nyingi tofauti. Hapa, tunaalikwa kufikiria matokeo ya ugonjwa na kifo juu ya familia, urafiki na jamii. Tunaona nini katika maandiko haya ambayo inaweza kutusaidia kufikiri juu ya jinsi ya kuwasaidia wale walio na Ebola?

Mistari ya kwanza ya sura ya 11 (vv1-14) inaonyesha wazi kwamba ugonjwa wa mtu haumufanyi kutengwa. Lazaro huleta wasiwasi kwa dada zake Marata na Maria; Swala la Yesu rafiki yake na Lazaro na watu walio karibu naye, pia shida inayofikia jamii ya Lazaro kule Betania inajitokeza katika mashairi haya.

**Maswali ya majadiliano**

*Fikiria kwamba mkristo wa kanisa lako anakuwa na homa kali na wakati wa kupimwa inaonyesha kwamba ana maambukizi ya Ebola. Chora mtandao (réseau) wa mahusiano yote ambayo mtu huyu anakuwa nayo ndani ya kanisa na jamii* (Ona mutandao hapa chini).

*Kama mtu wa ushawishi ndani ya jamii, ni hatua gani unaweza kuchukua ili kuwezesha ushirikiano bora wa watu badala ya uhusiano mbaya na magawanyiko kati ya watu.*
*Watu wanaweza kutaja kusaidia watu kukubali kuwa ugonjwa uko katikati yao, kuwa karibu na watu wa jamaa ya mutu aliyepatikana na ugonjwa, nk.*

Wakati ambapo Yesu anafika Betania, Lazaro alikuwa kaburini kwa siku ine. Yesu alipopita mujini, watu wengi walijua (v19 - 'Wayahudi wengi walikuwa wamekuja'). Kuja kwake pia kulikuja kujenga uhusiano kati ya yake na dada za Lazaro, Marata na Maria. Hawa dada zake, katika mazungumuzo na Yesu wanaweka lawama juu yake. Katika masemi yao, Yesu anajukumu katika yale yaliyotokea (angalia v21 na v32 'Bwana, kama ungekuwa hapa, ndugu yangu hangekufa.')

Yesu anakabiliwa na hali ambapo matokeo pekee yaliyofika inaonekana kuwa kifo, kupoteza, kilio na huzuni (vv38-39). Hakuna mtu anayetaka afungue kaburi. Hakuna mtu anayezani kwamba anaweza kufanya chochote. Hata hivyo katika hali hii Yesu anatumia uwezo wake kuleta uhai na uponyaji (vv40-44). Jiwe ambalo linafunga kaburi linaondolewa. Lazaro anaamuriwa kuondoka kaburini na kurejeshewa uhai.

***Maswali ya majadiliano***

*Katika mazingira ya Ebola, ni nini sababu (kama vile mashaka juu ya kuzikwa na ukingo ao unyanyaswaji wa wale wanaopona ugonjwa) zinazowaua watu katika jamii yako?*

*Watu wanaweza kutaja ujinga, uvumi, kutokuamini ukweli, nk.*

*Unawezaje kuungana na Yesu katika kupiganisha hizo sababu, kuziondoa na kuwezesha kurejeshwa kwa uhai kati ya watu.*

*Watu wanaweza kutaja mazungumuzo na mutu moja moja ao makundi madogomadogo.*



Lazaro anafufuliwa baada ya siku ine ya kufa (v44). Katika Injili, Lazaro ametajwa kuwa yeye na dada zake walimupa Yesu chakula cha jioni (Yohana 12: 1-7). Injili ya Yohana haionyeshe matokeo ya kifo hiki na ufufuko juu ya Lazaro ao dada zake. Ila, muujiza huu ulileta matokeo mengi katika jamii la Betania na mahali pengine (Yohana 12: 9-11 na Yohana 12: 17-19).

***Maswali ya majadiliano***

*Fikiria kile Lazaro, Marata na Maria walipashwa kusema juu ya matukio yanayoandikwa katika Yohana 11: 1-44.*

*Unafikiri wanaweza namna gani kukubaliana na huu ukweli kwamba Lazaro alikufa lakini akafufuliwa.*

*Unafikiri watu ambao wameambukizwa na Ebola (na familia zao) wanajisikia namna gani baada ya kupita katika magonjwa ya Ebola na wakapona (ao wakafa). Unafikiri watu hawa wanahitaji musaada wa aina gani?*

*Watu wanaweza kutaja kushukuru kwa uponyaji, kushuhudia makuu na maajabu ya Mungu, kufuatilia waiopona kisaikolojia, kiroho na kimwili, nk.*



**SOMO HIZI ZILISOMWA NA KUSAHIHISHWA KATIKA SEMINA YA WACHUNGAJI NA WAONGOZI WALIO CHINI YA UONGOZI WA KANISA LA KRISTO KATIKA KONGO.**

**WAHUZURIAJI WA SEMINA YENYEWE**

1. Mgr. Muhindo Nzayi Edmond, Evêque EPROBA CEBA et Modérateur ECC Ville de Butembo.
2. Rév Kambale Kilumbiro Martin, Vice-Président et Représentant Légal Suppléant de la Communauté Baptiste au Centre de l'Afrique, CBCA.
3. Dr Kakule Muyonga Isaac, Directeur du Département de la santé de la Communauté Baptiste au Centre de l'Afrique, CBCA.
4. Mr Polisi Kivava Jean Marie, Directeur du Déparement de Diaconie et Développement de la Communauté Baptiste au Centre de l'Afrique, CBCA.
5. Rév Kasereka Mukunyu, Pasteur évangéliste du poste Katwa de la Communauté Baptiste au Centre de l'Afrique, CBCA.
6. Rév Sivirwa Issembo Sem, Pasteur évangéliste du poste Kitsombiro de la Communauté Baptiste au Centre de l'Afrique, CBCA.
7. Rév. Kakule Taholokya Josias, Pasteur évangéliste du poste Kitsimba de la Communauté Baptiste au Centre de l'Afrique, CBCA.
8. Mr Mubere Yalala Isaac, Secrétaire de la Communauté des Eglises Pentecotistes en Afrique Centrale (CEPAC).
9. Rév Kasereka Ngororo, Pasteur évangéliste du poste Vayana de la Communauté Baptiste au Centre de l'Afrique, CBCA.
10. Rév Mathe Saa-Nane, Pasteur du secteur de Butembo de la Communauté des Eglises Baptistes au Congo-Est (CEBCE).
11. Rév Kambale Kanduvula, Pasteur de la Communauté Evangélique au Centre de l'Afrique (CECA20) à Butembo.
12. Rév. Mupagazi Bwanamuzuri, Coordinateur de l'évangélisantion de l'église Aglicane à Butembo.
13. Mme Masika Mwenge, Evangéliste de la Communauté des Eglises Pentecotistes en Afrique Centrale (CEPAC) de Beni.
14. Rév Kakule Kitamereka, Pasteur de la Communauté Evangélique au Centre de l'Afrique (CECA20) à Beni.
15. Rév Kavusa Ndungo, Pasteur évangéliste du poste Busaghala de la Communauté Baptiste au Centre de l'Afrique, CBCA.
16. Evangéliste Mutabazi Mathe, Evangéliset au sein de l'Eglise du Christ au Congo, ville de Beni.
17. Rév Maseku Mayao, Pasteur évangéliste du poste Beni de la Communauté Baptiste au Centre de l'Afrique, CBCA.
18. Rév Kambale Muviswa, Pasteur de la Communauté Baptiste au Centre de l'Afrique, CBCA à Butembo.
19. Rév Kavusa Sivitsomwa, Pasteur évangéliste du poste Maboya de la Communauté Baptiste au Centre de l'Afrique, CBCA.
20. Rév Katembo Kitaheruka, Pasteur évangéliste du poste Buyinga de la Communauté Baptiste au Centre de l'Afrique, CBCA.
21. Rév Kambale Sibangeha John, Pasteur évangéliste du poste Bwatsinge de la Communauté Baptiste au Centre de l'Afrique, CBCA.
22. Rév Kambale Mukanirwa Etienne, Pasteur de la Communauté Baptiste au Centre de l'Afrique, CBCA à Beni.
23. Rév Katsuva Vamukwamire, Pasteur évangéliste du poste Kisima de la Communauté Baptiste au Centre de l'Afrique, CBCA.
24. Nimwenge Mbindule, Présidente de la jeunesse de la Communauté Baptiste au Centre de l'Afrique, CBCA à Butembo.
25. Rév Mbusa Muke Steven, Pasteur évangéliste du poste Mambowa de la Communauté Baptiste au Centre de l'Afrique, CBCA.
26. Rév Muhindo Kombi, Pasteur évangéliste du poste Bambo de la Communauté Baptiste au Centre de l'Afrique, CBCA.

27. Mr Olivier Kaskoti, Directeur de la Radio de l'Eglise du Christ au Congo, ville de Beni.
28. Rév Dr Kavasya Kule, Directeur de l'Institut Biblique de Katwa appartenant à la Communauté Baptiste au Centre de l'Afrique, CBCA.
29. Mr Kalebu Vihugho, Pasteur de la Communauté Baptiste au Centre de l'Afrique, CBCA à Beni.